

102/3

KISWAHILI

FASIHI

KARATASI YA 3

JULAI / AGOSTI 2014

MUDA : SAA 2 ½

MTIHANI WA MWIGO WA KAUNTI NDOGO YA HOMA-BAY
Hati ya kuhitimu kisomo Sekondari Kenya(KCSE)

102/3

Kiswahili

Karatasi ya 3

Saa 2 ½

MAAGIZO:

- *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
- *Jibu maswali manne pekee.*
- *Swali la kwanza ni lazima.*
- *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizosalia yaani; (Riwaya, Hadithi fupi, Tamthilia na, fasihi simulizi.*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*
- *Kila swali lina alama 20*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI :-

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	80	

Karatasi hii ina kurasa 3 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

SEHEMU YA A
FASIHI SIMULIZI

Swali Ya Lazima

1. (a) Maigizo ni nini? (al.2)
(b) Taja vipera vyovoyote vili vya maigizo (al.10)
(c) Eleza dhima zozote tano za maigizo (al.10)
(d) Jadili njia zinazotumiwa na kizazi cha sasa kuendeleza utanzu huu. (al.6)

SEHEMU YA B RIWAYA :

KIDAGAA KIMEMWOZEA : Ken Walibora

2. “Nilikwambia twende ukakataa.....si kuona, tuone ndipo tuambe”
(a) Weka dondo katika muktadha wake (al.4)
(b) Fafanua hulka za mswemewa (al.6)
(c) Taja tamadhali ilitumika katika dondo (al.2)
(d) Eleza umuhimu wa yanayorejelewa (al.4)
(e) Jadili umuhimu wa msomaji (al.4)
3. “Nchi ya Tomoko imejawa na uozo” tetea kauli hii kwa mujibu wa riwaya ya kidagaa kimemwozea (al.20)

SEHEMU YA C TAMTHILIA:

MSTAHIKI MEYA

4. Fafanua mbinu walizotumia wanacheneo kujikomboa (al.20)
5. “...kina raha gani watoto wetu wanapofukuzwa shule kwa sababu hatuwezi kuwalipia karo?
kuna raha gani.....
(a) Weka dondo katika muktadha wake (al.4)
(b) Eleza sifa za msemewa (al.4)
(c) Jadili umuhimu wa msemaji (al.2)
(d) Dondoo limetumiwa tamathali zipi? (al.4)
(e) Wanacheneo wamezonga na matatizo mengi tetea kauli hii kulingana na tamthilia (al.6)

SEHEMU YA D HADITHI FUPI:

DAMU NYEUSI (Ken Walibora S. Mohamud)

6. Jadili maswala ibuka ukirejelea visa viNne kutoka kwa hadithi zifuatazo
(i) Mke wangu
(ii) Samaki wa nchi za joto
(iii) Damu nyeusi
(iv) Gilasi ya mwisho makaburini
7. “.....Nani kakwambia kwamba mimi unanihusudu”
(a) Weka dondo katika muktadha wake (al.4)
(b) Ni nini dhamira ya kisa kinachotajwa? (al.2)
(c) Kisa kinachorejewa kinaakisi jamii ya kisasa. Tetea (al.10)
(d) Msanii Mohamed Ghassanyamefanikiwa kutumia kinaya. Tetea kwa mifano minne (al.4)

SEHEMU VYA E USHAIRI

8. VITA VYA NDIMI

Huyo !Amshike huyo !
 Hakuna bunduki wala kifami
 Bomu na risasi hata hawazijui
 Lakini mno wanashambuliana
 Kwa ndiMi zilizonolewa kwa makali
 Vipande vya matusi silaha zao

Yu imara mmoja wao
 Akirusha kombora la nenO zito!
 Litingishe adui wake
 Na kungusa hisia kwa pigo kuu
 Pigo linalochoma moyoni kama kichomi
 Kuchipuza joto la hasira na kisasi
 Katika mapigano yaso na kikomo

Filimbi ya suluhu inapulizwa kuwaamua!
 Ni nai anayekubali suluhu?
 Roho zinakataa katakata
 Huku ukaidi ukinyemelea na kutawala kote
 Mapandikizi ya watu yakiigana
 Vita shadidi visivyo ukomo
 Vita vya ndimi!

Magharibi sasa
 Jua linapungia mkono machweo
 Nalo giza likinyemelea kwa kiburi na
 Kasi
 Sisikii tena sauti za mIsongo
 Mate ya watesi yamekauka
 Makanwa yao yamelemewa na uchovu
 Sasa wameshikana mikono
 Ishara ya suluhu

Maswali

- (a) Hili ni shairi la aina gani? (al.1)
- (b) Eleza dhamira ya mshairi (al.2)
- (c) Eleza siFa za utunzi alizotumia mshairi (al.3)
- (d) Taja tamathali zozote tatu alizotumia mshairi (al.3)
- (e) Eleza toni ya mshairi katika beti tatu za awali (al.1)
- (f) Eleza hatima ya yanayozungumziwa kwenye shairi (al.1)
- (g) Mshairi ametumia alama hisi kwingi. Eleza umuhimu wake (a.1)
- (h) Itambue nafsi neni katika shairi (al.1)
- (i) Andika mishororo ya kwanza mitatu ubeti wa 4 kwa lugha ya nathari (a.3)
- (j) Toa maana ya msamiati huu (al.2)
 - (i) Kombora
 - (ii) Misonyo

9.

Ndege mwema na muruwa, katu haishi tunduni
Hataki kufadhiliwa, muda yumo utumwani
Japo mnyonyoe mbawa, mwisho wake utahuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege ataka yoyoma, nasiyahi msituni
Apite akisimama, shinani na mitawini
Haridhiki kwa mtama, na maji ya kikombeni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa hishma mwema mno wa kughani
Tundu huliona chama, japo liwe la thamani
Huporomosha yakwe kima, na kufanya faraghani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mpambe kwa zari, na lulu na marijani
Upambe yake suduri, kwa almasi kidani
Tunduni atahajiri, ili awe huriani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa busara, hatoishi kifungoni
Anayo kubwa hasara, kukosa nyumba ya mani
Lamkera lamkera, tundu la dhahabu kwani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege maumbile yake, na waja hayalingani
Yeye hutaka wenzake wafukuzane hewani
Jambo la kuishi pweke, kamwe humridhiani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Baiti zangu ni haba, nakonea kituoni
Ndege huficha mahaba, kama yumo kifungoni
Hali ndege akashaba, kwani yumo adhabuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Maswali

- | | |
|---|--------|
| (a) Lipe shairi anwani mwafaka | (al.1) |
| (b) Fumbua maana ya ndege anayerejelewa | (al.1) |
| (c) Shairi hili ni la mkondo gani? | (al.3) |
| (d) Eleza muundo wa ubeti wa nne | (al.3) |
| (e) Fafanua uhuru aliotumia mshairi | (al.4) |
| (f) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari | (al.4) |
| (g) Jadili dhamira ya mshairi | (al.2) |
| (h) Fafanua maana ya msamiati ufuatao kama ulivytumiwa na mshairi | (al.2) |
| (i) Alahuni | |
| (ii) Baiti | |